Learning on TAP

# Upimaji wa uoni na usikivu kwa watoto wa umri wa shule

Jumbe muhimu: Utangulizi kuhusu upimaji wa milango ya fahamu (sensory screening)

## Somo la kwanza: Utangulizi kuhusu upimaji wa milango ya fahamu

### Uoni na usikivu

Ili kuweza kuona na kusikia vizuri, ni muhimu macho na masikio yote mawili kuweza kufanya kazi vizuri na kuwa na afya njema. Uoni na usikivu vinasaidia watoto kwa njia mbali mbali. Matatizo katika kuona na kusikia yanaweza kuathiri uwezo wa mtoto kujifunza na kushiriki katika shughuli za kila siku. Hii inaweza kuathiri maisha yao ya nyumbani, na masomo shuleni pamoja na kufanikiwa kimaisha wakati wa utu uzima.

Watoto anaweza kuwa na matatizo ya kuona, kusikia au yote mawili. Matatizo haya yanaweza kutokea kutokana na sababu nyingi, ikiwemo magonjwa au changamoto za kiafya, maambukizi ya macho au masikio, kuharibika kwa macho au masikio. Matatizo mengi ya kiafya ya macho yanaweza kuepukika au kupunguzwa kwa kutumia mabadiliko katika mfumo wa maisha, matibabu, vifaa saidizi na/ au huduma za kutengamaa.

Kuongeza uelewa kwa watoto, famillia na walimu kuhusu umuhimu wa afya ya macho na masikio, pamoja na kuhamasisha ushiriki wa jamii kwenye huduma; ni mambo muhimu kwenye kufanikisha kinga na huduma.

### Upimaji wa milango ya fahamu

Upimaji wa hisia hizi unajumuisha vipimo vidogo vidogo vidogo ili kujua kama mtoto anaweza kuwa na:

Tatizo la kuona na/au kusikia
Tatizo la kiafya la macho au masikio

Upimaji hauthibitishi ugonjwa, wala tatizo. Upimaji uainisha kama mtoto anahitaji kupewa rufaa kwwenda kumuona mtaalum aliyepata mafunzo ya macho na/ au masikio kwa ajili ya hatua zaidi.

Upimaji wa milango ya fahamu unahusisha kupata ridhaa ya mtu anayepimwa,kufanya upimaji na kutoa rufaa kwa mtoto kama itahitajika kufanya hivyo. Upimaji unaweza kusaidia:

Kuanisha matatizo ya Uoni na usikivu mapema kabisa kwenye maisha ya mtoto
Kutoa rufaa kwenda kupata huduma nyingine haraka, ili kuzuia uharibifu wa Uoni na usikivu
Kuepuka au kupunguza ahari hasi za matatizo ya hisia za uoni na usikivu kwenye maisha ya mtu.

Watoto wanapaswa kufanyiwa upimaji wa milango ya fahamu wanapoanza shule na kila baada ya mwaka1 hadi 2. Wakati mwingine Upimaji wa Uoni na usikivu hufanyika katika maeneo tofauti.Hatahivyo, upimaji wa pamoja ni bora zaidi. Upimaji wa pamoja unaweza:

- Tambua matatizo ya uoni na/au kusikia mapema kabisa katika maisha ya mtoto.
- Inapunguza gharama na muda

## Somo la pili: Ufanyaji programu ya upimaji kwa Watoto wa Umri wa Shule

### Uaandaji wa programu ya kupima

Kabla ya kutekeleza programu ya kupima, ni muhimu:

- Kupata idhini kutoka kwa Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu
- Kuanisha sehemu za upimaji zenye uwezo wa kufanya programu za upimaji, ikiwemo wafanyakazi pamoja na mazingira yanayofaa.
- Kuainisha njia za kutoa rufaa na taratibu za huduma za macho na masikio
- Kuainisha na kutoa mafunzo kwa wanaotoa huduma ya upimaji
- Kifaa cha upimaji

**Mambo ya kuzingatia kwenye kujumuisha**

Watoto **WOTE** wanapaswa kuwa una uwezo wa kufanyiwa upimaji . Hii inajumuisha watoto ambao wanajulikana kuwa na matatizo ya Uoni na usikivu na wale wenye mahitaji ya kimaumbile na kujifunza.

Jadili pamoja na maratibu wa upimaji wa shule namna bora yakufanya upimaji kwa watoto wote wenye mahitaji ya ziada na wekeni mpango wa kuitekeleza.

Kabla ya kufanya upimaji wa milango ya fahamu, ni muhimu kupata ridhaa kwa kila mtoto kutoka kwa mtu aliyeidhinisha kutoka ridhaa hiyo. Mtu huyu anaweza kuwa wazazi/ mlezi au mkuu wa shule. Kama ridhaa haikutolewa, mratibu wa upimaji anapaswa kuongea na mzazi/mlezi ili kujaribu kupata sababu ya uamuzi huo. Wazazi wanaweza kuhitaji taarifa zaidi au kuhakikishiwa zaidi kuhusu usalama wa kipimo hicho.

**Maandalizi ya kipimo**

Maandilizi yanajumuisha:

- Kuaandaa eneo na vifaa
- Kutayarisha nyaraka
- Kuanda mpango wa utaratibu wa upimaji
- Kipindi cha maandalizi ya kikundi ili kuandaa waoto watakaofanyiwa kipimo

**Itakapofika mwisho wa siku ya upimaji**

Hakikisha nyaraka zote zimekamilishwa ikiwemo:

- Rejesta ya mahudhurio
- Fomu za upimaji ili kurekodi matokeo ya upimaji
- Orodha ya ufuatiliaji wa rufaa kurekodi watoto wanaohitaji mtoa huduma ya afya ya macho na/au masikio

Unapaswa pia kusafisha sehemu ya upimaji na kifaa cha upimaji

**Baada ya siku ya upimaji**

Baada ya siku ya upimaji, mpimaji na mratibu wa upimaji wa shuleni :

- Watawataarifu wazazi/ walezi matokeo ya upimaji
- Watawasiliana na watoa huduma wanaotarajia kupokea rufaa ili kuwajulisha idadi ya watu wanaweza kutarajia.
- Kufanya ufuatiliaji ili kujua kama wale waliopewa rufaa wamekwenda kweli kupata huduma
- Kupanga siku ya kufanya ufuatiliaji kwa watoto ambao hawakuweza kupimwa

Ni muhimu kutunza kumbukumbu zote na sahihi, kwa vile zitatumika kusimamia na kutathimini namna programu inavyoendeshwa

**Somo la tatu: Rufaa kwa mtaalamu wa huduma ya macho na masikio**

Mahudhurio ya watoto kwenye maeneo waliopewa rufaa kwenda kuonana na wataalamu ni muhimu ili kuepuka au kupunguza athari hasi za matatizo ya hisia za uoni na usikivu kwenye maisha ya mtoto. Wazazi/walezi wanapewa taarifa kuhusu mahali pa kupeleka mtoto kwa kutumia fomu ya kutoa taarifa.

Programu nyingi za upimaji hazifanikiwi kwasababu watoto hawapelekwi kwenye miadi inayofuatia. Njia za kusaidia kuboresha mahudhurio kwenye miadi inayofuatia inajumuisha:

- Kufuatilia rufaa ili kusimamia mahudhurio kwa miadi inayofuatia
- Kuwasaidia wazazi kwa kuainisha vikwazo vya kupeleka watoto kwenye miadi na kudodosa suluhisho la vikwazo hivyo